



**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA
BORA**

**Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere - Kilimani
S.L.P 1049, DODOMA**

Simu: +255 734 047 775; 734 119 978

Barua Pepe: info@chragg.go.tz

Tovuti: www.chragg.go.tz

Mei 01, 2020

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI
Salamu za Pole kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John
Pombe Magufuli.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imepokea kwa mshituko mkubwa taarifa za kifo cha aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb) kilichotokea leo alfajiri Mei 01, 2020 Jijini Dodoma.

Tume inatoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuondokewa na kiongozi mchapakazi, mwadilifu, mzalendo na mwanadiplomasia mahiri aliyeiwakilisha na kuipigania Tanzania katika nyanja za Kimataifa kwa miaka mingi.

Aidha, Tume inatoa salamu za pole kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Job Yustino Ndugai, Wabunge, Wafanyakazi wa Wizara ya Katiba na Sheria, familia ya Marehemu na wananchi wa Mkoa wa Iringa kwa kuondokewa na mpendwa wao.

Tume ikiwa taasisi iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria inaungana na Watanzania wote katika kuomboleza msiba huu na inawaomba wanafamilia wote kuwa na moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahala pema peponi, Amina.

Imetolewa na:



Jaji (Mst) Mathew Pauwa Mhina Mwaimu

Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Mei 01, 2020